

Dhima za Kialami Pragmatiki ‘mh’ katika Mazungumzo ya Kiswahili

Magreth J. Kibiki
Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

kibiki65@gmail.com

na

Pendo S. Malangwa
Profesa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

psmalangwa@gmail.com

Ikisiri

Makala hii inachunguza dhima za kialami pragmatiki *mh* katika mazungumzo ya Kiswahili. Data ya makala hii imekusanywa kutoka katika mazungumzo yasiyo rasmi ya Kiswahili yanayofanywa katika maeneo yasiyo rasmi. Maeneo hayo ni kama kwenye vijiwe vya kahawa na vijiwe vya mamantilie. Uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Umuktadhaishaji ya Gumperz (1982). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kialami pragmatiki *mh* huchanua maana tofautitofauti kulingana na muktadha kinamotumika. Kwa hiyo, kialami pragmatiki hicho huwa na dhima mbalimbali za kipragmatiki. Baadhi ya dhima hizo ni kama vile kuashiria kuitika, kumtaka mzungumzaji arudie kauli au swali, kumjulisha mshiriki mwingine wa mazungumzo apokee au achukue kitu, kudokeza kwamba mzungumzaji anaanzisha mazungumzo, kumruhusu mzungumzaji mwingine aendelee kuzungumza, kutumika kama jibu la swali na kuonesha hisia mbalimbali kama vile dharau na mshangao. Kwa ujumla, makala hii inaadokeza kwamba vialami pragmatiki vina dhima mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, tafiti zaidi zifanyike ili kubaini dhima za vialami pragmatiki vingine katika lugha hii. Aidha, kialami pragmatiki *mh* kinaweza kuchunguzwa zaidi kwa kuhusisha na taaluma za fonolojia na fonetiki ili kubaini ruwaza zake na athari zake kwenye maana za kialami hicho.

Dhana za Msingi: Kialami, pragmatiki, lugha ya mazungumzo

Utangulizi

Fasili ya dhana ya vialami pragmatiki (kuanzia sasa VIPRA) ni tata kwani mpaka sasa hakuna fasili moja inayotumiwa na wanaisimu wote wanapovirejelea. Schiffrin (1987) anafasili VIPRA kuwa ni vipashio vya usemaji vinavyofungua au kufunga usemi. Fasili hii ya Schiffrin (1987) inazua utata kwani haiweki bayana vipashio anavyovirejelea. Pia, imezingatia zaidi vipashio vinavyowekwa mwanzoni au mwishoni mwa usemi tu (vinavyofunga au kufunga usemi) na kuacha vile vinavyoweza kuwekwa katikati ya usemi. Tofauti na Schiffrin (1987), Redeker (1991) anafasili VIPRA kwamba ni neno au kirai ambacho hutamkwa kwa lengo la kumfanya msikilizaji awe makini juu ya uhusiano baina ya kinachosemwa sasa na kitakachosemwa baadaye (S1 na S2) katika kilongo cha mazungumzo. Fasili hii ya Redeker (1991) imetusaidia kubaini kwamba KIPRA kinaweza kuwa neno au hata kirai na dhima yake ni kuweka uhusiano baina ya sentensi katika kilongo cha mazungumzo. Hata hivyo, fasili yake imemuegemea msikilizaji peke yake ilhali VIPRA vinamsaidia pia msemaji kuelewa ikiwa mshiriki mwingine wa mazungumzo anafuatilia kinachosemwa.

Naye Fraser (1999) anafasili VIPRA kwamba ni maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia kama vile viunganishi, vielezi na virai vihusishi ambavyo huashiria uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na ya awali (S2 na S1). Anasisitiza kwamba VIPRA huwa na maana zake za msingi ambazo ni za kimchakato na maana zake za ziada ambazo hutegemea muktadha wa matumizi. Tukizichunguza fasili za Redeker (1991) na Fraser (1999), tunaona kwamba wataalamu hawa wanakubaliana

kwamba VIPRA vinaweza kuwa maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia, lakini wanatofautiana katika kuelezea suala la uhusiano unaodhihirishwa na VIPRA baina ya sentensi. Wakati Redeker (1991) anaona VIPRA hudhihirisha uhusiano baina sentensi inayosemwa sasa na itakayosemwa baadaye (S1 na S2), Fraser (1999) anaona VIPRA huonesha uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na iliyosemwa awali (S2 na S1). Utata huu unazongolewa katika fasili ya Van Bergen na Degend (2018) ambao wanafafanua kwamba VIPRA hudhihirisha uhusiano baina ya sentensi inayosemwa sasa na sentensi iliyosemwa/zilizosemwa kabla au baada ya hiyo inayosemwa sasa katika kilongo cha mazungumzo.

Japokuwa fasili za Redeker (1991), Fraser (1999) na Van Bergen na Degend (2018) zimetusaidia kuelewa juu ya dhana ya VIPRA, bado haziweki wazi nafasi ambazo VIPRA hukaa katika sentensi. Kwa upande mwingine, Fung na Carter (2007) wanafasili VIPRA kwamba ni vipashio vya kiisimu ambavyo huweza kupachikwa ndani au nje ya sentensi (mwanzoni, katikati au mwishoni mwa sentensi) katika mazungumzo ili kujenga uhusiano baina ya matamko na kudhihirisha ushirikiano katika mazungumzo baina ya mzungumzaji, msikilizaji na ujumbe unaowasilishwa. Anasisitiza kwamba VIPRA huwa ni vya hiari. Hii ina maana kwamba huweza kuondolewa katika muktadha wa sentensi bila kubadili maana ya msingi ya sentensi hiyo na wala kuathiri masharti-ukweli ya sentensi husika. Tofauti na fasili zilizotolewa na Redeker (1991), Fraser (1999), Van Bergen na Degend (2018), Fung na Carter (2007) wanatumia istilahi ya tamko badala ya sentensi. Hii ina maana kwamba VIPRA havitumiki tu kuashiria uhusiano baina ya sentensi, bali huweza kuashiria uhusiano baina ya matamko katika kilongo cha mazungumzo. Tamko katika muktadha huo

linaweza kuwa neno, kirai, kishazi, sentensi, na aya. Licha ya kutofautiana katika fasili zao, Redeker (1991), Fraser (1999), Fung na Carter (2007) na Van Bergand na Degand (2018), wanakubaliana kwamba VIPRA vina dhima nyingi na ni vya aina nyingi. Wanasisitiza kwamba VIPRA huwa na maana zake za msingi, lakini huweza kuchanua maana mbalimbali kutegemeana na muktadha wa matumizi katika tamko linalohusika. Kwa kuzingatia ufafanuzi wa wataalamu hawa na kwa kuzingatia VIPRA katika lugha ya Kiswahili, kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba VIPRA ni maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia kama vile: vielezi, viunganishi, vitenzi, vihisishi na virai vihusishi. Dhima ya maneno au virai hivyo ni kusaidia kumueleweshwa mshiriki wa mazungumzo kufasiri uhusiano baina ya tamko linalosemwa sasa na lililosemwa kabla au baadaye katika kilongo cha mazungumzo. VIPRA huwa na maana zake za msingi (wakati mwingine havina kabisa maana hiyo). Maana hizo hutajirishwa na muktadha vinamotumika, na, hivyo, kuwa na dhima mbalimbali za kipragmatiki. Aidha, dhima zake hutegemea nafasi yake katika tamko, kiimbo kilichotumika na viziada lugha vilivyoambatana na usemaji wa VIPRA hivyo.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu VIPRA katika lugha ya Kiswahili (Taz. Suzan, 1990; Kibiki na Malangwa, 2018, 2019a, 2019b; Kibiki, 2019a, 2019b; Goodness, 2020; Marjie na Sosoo, 2021). VIPRA vilivyochunguzwa kutokana na tafiti hizo ni kama vile *sasa*, *basi*, *maana*, *haya*, *kumbe*, *sawa*, *eh* na *ah*. Matokeo ya tafiti kama vile za Kibiki (2019a, 2019b) yanaonesha kwamba upo uwezekano wa dhima za VIPRA kutofautiana. Hii ina maana kwamba, licha ya ufanano, kila KIPRA kina upekee wake katika kuchanua dhima zake. Hivyo, ni wazi kwamba ipo haja ya kuchunguza VIPRA

vingine katika lugha hii ili kubaini dhima zake. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza dhima za KIPRA *mh* katika mazungumzo ya Kiswahili. KIPRA *mh* kiliteuliwa kwa sababu uchunguzi wa awali uliofanywa na watafiti unaonesha kwamba kina tabia ya kuchanuza dhima nyingi kinapotumiwa katika muktadha wa mazungumzo ikilinganishwa na VIPRA vingine vya Kiswahili ambavyo bado havijafanyiwa uchunguzi.

Sababu nyingine ya uteuzi wa KIPRA hiki ni kwamba hakijapewa umuhimu kiutafiti si tu katika lugha ya Kiswahili, bali hata katika lugha nyinginezo duniani. Kwa ufahamu wetu, tafiti zilizofanywa kuhusu KIPRA *mh* ni zile za Pipek (2007), BAKIZA (2010), TUKI (2012), BAKITA (2017) na Kibiki (2019b). Pipek (2007) amechunguza KIPRA *mh* katika lugha ya Kiingereza na anabainisha kwamba KIPRA hicho kina dhima ya kipragmatiki ambayo ni kumueleweshwa mshiriki wa mazungumzo kwamba msikilizaji yupo pamoja na mzungumzaji, hivyo, aendeleo kuzungumza. Hata hivyo, utafiti wa Pipek (2007) umedokeza dhima moja tu ya KIPRA *mh*. Hii pengine ni kwa sababu utafiti wake haukukusudia kuchunguza dhima nyingine za KIPRA hicho kwani utafiti wake ulikitwa kuchunguza VIPRA vya usikizi kwa ujumla. Aidha, utafiti wa Pipek umedokeza kuhusu KIPRA *mh* katika lugha ya Kiingereza huku wetu ukiangazia dhima mbalimbali za kipragmatiki za KIPRA *mh* katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, tafiti za BAKIZA (2010), TUKI (2012) na BAKITA (2017) zinatoa ufafanuzi wa kisemantiki, yaani maana msingi ya KIPRA hicho. Hatupati ufafanuzi wa kipragmatiki kuhusu dhima za KIPRA *mh* katika muktadha wa mazungumzo. Aidha, utafiti wa Kibiki (2019b) umejikita katika kuchunguza mchango wa ishara za mwili kwenye maana ukitumia VIPRA *eh*, *sawa*, *mh* na *ah* kama uchunguzi kifani. Kwa kuwa

halikuwa lengo la utafiti huo kufafanua kwa kina dhima mbalimbali za KIPRA *mh*, bado tunakosa ufafanuzi huo muhimu. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuchunguza zaidi kuhusu dhima za kipragmatiki za KIPRA *mh* katika mazungumzo ya Kiswahili na hilo ndio lengo hasa la makala hii.

Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuktadhaishaji iliyoasisiwa na John Gumperz (1982). Nadharia hii inaitazama maana kama kitendo kinachorekebisha na muktadha na kinachorekebisha muktadha pia. Kwa mujibu wa Gumperz, matamko hukitwa katika muktadha ambao hufanikisha na kurahisisha mchakato mzima wa kubaini maana za matamko hayo. Gumperz anasisitiza kwamba ingawa tunashughulikia matamko yenye miundo iliyopangiliwa ili kuwasilisha kile tunachokikusudia, miundo hiyo si tuami bali hurekebisha na kuafikiwa katika mchakato mzima wa mawasiliano. Hivyo, maana haiukiliwi na kile kinachosemwa tu, bali kwa kuzingatia namna tamko hilo linavyotumiwa katika muktadha husika.

Kwa mujibu wa nadharia hii, tamko linaweza kupata maana tofautitofauti kulingana na namna wazungumzaji wanavyolitumia katika muktadha mahususi. Ili kung'amua maana ya kinachosemwa, nadharia hii inasisitiza zaidi kuzingatia viashiria mbalimbali vya kimuktadha. Viashiria vya kimuktadha, kwa mujibu wa Gumperz (1982), vinajumuisha vipengele mbalimbali vya lugha. Vipengele hivyo ni kama vile vya kiisimu (mfano, maneno yaliyotumika, mpangilio wa vipashio katika sentensi, uhusiano baina ya tamko moja na jingine na maana za msingi za matamko hayo), mada, viziada lugha kama vile viarudhi (mfano, kiimbo, mkazo na kidatu) na matendo na ishara mbalimbali za mwili (kama vile mwonekano wa macho, sura na pingiti). Kwa mujibu wa nadharia hii, viashiria hivi vya

kimuktadha vinachukuliwa kama malighafi za kisemiotiki zinazosaidia kuchanua maana. Wazungumzaji hutumia viashiria hivyo vya kimuktadha kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusiana na kile wanachokikusudia wasikilizaji wakifasiri. Hivyo, maana ya kile kinachosemwa hutegemea jitihada za washiriki wa mazungumzo kutumia viashiria mbalimbali vya kimuktadha ili kumwelevesha msikilizaji kile wanachokusudia kukipa umuhimu zaidi kuliko kingine. Nadharia hii ilituliwa kwa sababu dhima za KIPRA *mh* zimekitwa katika muktadha wa mazungumzo, jambo ambalo linasisitizwa pia na nadharia hii. Hivyo basi, dhima mbalimbali za KIPRA hicho zimefafanuliwa kwa kuzingatia viashiria mbalimbali vya kimuktadha. Viashiria hivyo ni kama vile nini kimesemwa kabla au baada ya kutumia KIPRA *mh*, kiimbo kilichotumika, nafasi kinamokaa katika tamko, vitendo na ishara za mwili zilizoambatana na usemaji wa KIPRA hicho.

Ingawa nadharia hii inatambua kiimbo kama kiashiria kimojawapo cha kimuktadha kinachosaidia kubaini maana, haiweki bayana kiimbo hasa ni nini. Wataalamu kama vile Halliday (1994), na Snow na Balog (2002) wanakiri kwamba si rahisi kusema kiimbo hasa ni nini kwa sababu kinaonekana kuwa ni dhana changamani inayohusisha vipengele mbalimbali vya lugha kama vile sarufi, pragmatiki, na masuala ya hisia. Hali hii imesababisha kuibuka kwa pande mbili za wataalamu wenye mawazo yanayosigana kuhusu dhana ya kiimbo. Wapo wanaisimu wanaofasili kiimbo kuwa ni umbo-sauti linalotokana na mpando-shuko wa sauti za maneno wakati wa usemaji (Taz. Kwa mfano Kreidler, 2002; Massamba na wenzie, 2013). Tukiichunguza fasili hii tunabaini kwamba wataalamu hawa wanafafanua kiimbo kwa kujikita katika taaluma za

fonolojia na fonetiki. Kwa mujibu wa fasili hiyo kiimbo huweza kuwa ama cha chini, cha kati au cha juu.

Kwa upande mwingine, wanaisimu kama vile Egan (1980), na Baumann na Grice (2006) wanafafanua kiimbo kwa mwelekeo wa taaluma ya pragmatiki. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, fasili ya kiimbo inayohusisha mpando - shuko wa mawimbi ya sauti ni fasili finyu ya kiimbo. Kwa hiyo, wanafasili kiimbo kuwa ni namna tofautitofauti za kusema neno au mfululizo wa maneno. Wanafafanua kwamba fasili hii ni pana kwani, licha ya kiimbo kuhusisha mpando -shuko wa mawimbi ya sauti, kinajumuisha pia vipengele vingine vya kimsikiko kama vile mkazo, kidatu, urefushaji wa silabi na kadhalika. Hivyo, kutokana na fasili hii tunaweza kuwa na viimbo kadha wa kadha kama vile viimbo vya huzuni, viimbo vya hasira na hata viimbo vya mshangao. Kwa hiyo, licha ya kuongozwa na Nadharia ya Umuktadhaishaji ya Gumperz (1982), makala hii imeongozwa pia na fasili ya kiimbo kwa mujibu wa Egan (1980) na Baumann na Grice (2006). Sababu ya kuteua fasili ya wataalamu hawa ni kwamba ufafanuzi kuhusu athari za kiimbo kwenye dhima za KIPRA *mh* katika utafiti huu umekitwa zaidi katika taaluma ya pragmatiki. Kwa ujumla, watafiti wameonesha katika mjadala wa matokeo ya utafiti huu dhima mbalimbali za KIPRA *mh* zikichanuzwa kwa kuzingatia ushahidi unaopatikana ndani ya mazungumzo ya Kiswahili katika muktadha halisi.

Methodolojia

Utafiti huu ni wa uwandani. Ulifanywa kuanzia Novemba 2019 mpaka Januari 2020. Data zilikusanywa kutoka katika mazungumzo yasiyo rasmi yanayofanyika katika vijiwe vya kahawa na vya mamantilie. Eneo la utafiti lililotumika kupata data ya utafiti huu ni Mkoa wa Dar es Salaam katika

Wilaya ya Ubungo, Kata ya Manzese na Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Tanga-Mjini, Kata ya Ngamiani-Kati. Jumla ya vijawe 20 (Vijawe 10 kutoka kila kata) vilitumika kupata data. Idadi hii ilituliwa kwa sababu iliwezesha kupata data toshelevu, halisi na inayoakisi matumizi ya VIPRA katika lugha kwa ujumla. Kwa kila kata, vijawe vitano vilikuwa vya kahawa na vijawe vitano vya mamantilie. Ili kupata data kutoka katika vijawe hivyo, mbinu ya ushuhudiaji-shiriki ilitumika (Kawulich, 2006). Kwa kutumia mbinu hiyo, mazungumzo yaliyofanyika katika vijawe vya kahawa na vya mamantilie yaliweza kurekodiwa kwa kutumia kinasa sauti. Vilevile, kumbukumbu mbalimbali kuhusu matendo na ishara za mwili zilizoambatana na mazungumzo hayo vilirekodiwa katika shajara.

Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaielezo (Kreswell, 2014) na kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa vilongo (Ponera, 2019). Uchambuzi huo ulifanywa kwa kufuata hatua zifuatazo: Mosi, mazungumzo yote yalikusanywa na kuhifadhiwa katika sidii. Baada ya hatua hiyo, yalisikilizwa kwa umakini, kwa kurudia mara kwa mara na kuteua mazungumzo ambayo yana data iliyokusudiwa. Hatua hiyo ilifuatiwa na mchakato wa unukuzi wa mazungumzo hayo. Unukuzi wa mazungumzo ulifanywa kwa kutumia mfumo wa unukuzi wa Jeffersonian kama unavyoelezwa na Psathas na Anderson (1990) (Taz. Kiambatisho). Hata hivyo, alama za unukuzi kutoka katika mfumo huo hazikukidhi mahitaji yote ya unukuzi. Kwa hiyo, watafiti walibuni alama nyingine ili kukidhi mahitaji ya data walizozipata uwandani. Baada ya kufanya unukuzi, watafiti walifanua dhima za KIPRA *mh* katika mazungumzo ya Kiswahili wakiongozwa na Nadharia ya Umuktadhaishaji ya Gumperz (1982).

Matokeo ya Utafiti

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kutoka kwenye mazungumzo yaliyofanyika katika vijiwe vya mamantilie na vijiwe vya kahawa, imethibitika kwamba KIPRA *mh* kina dhima anuwai za kipragmatiki. Ufafanuzi kuhusu dhima hizo umetolewa katika sehemu zinazofuata.

Dhima ya kuitika

KIPRA *mh* kilibainika kuwa na dhima ya kipragmatiki ambayo ni kuitika. Dondoo Na. 1 kutoka katika mazungumzo yaliyofanyika katika kijiwe kimojawapo cha kahawa inathibitisha dhima hii:

Dondoo Na. 1:

1. A. ... ((Anaita)) Bwana Majaliwa.
 2. B. ↑**M::h**↓((anaitika))
 3. A. Uliangalia ile ‘mechi’ ya jana?
 4. B. Naachaje kuangalia.
 5. A. Uliona namna tulivyowachakaza? Mi nilishakwambia YANGA safari hii ni kichapo tu.
 6. B. Āh wapi::, goli lenyewe mlipata kwa kubahatisha tu vinginevyo tungewafunga sisi.
 7. A. ha ha ha mpira hauna bahati. Mpira ni mazoezi bwana...
- Chanzo:** Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Tanga (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, mzungumzaji A anaonekana kumwita mzungumzaji B, na mzungumzaji B anaitika kwa kutumia KIPRA *mh*. Baada ya kuitika, mzungumzaji A anaendelea kuzungumza kile alichokikusudia (anauliza kama mzungumzaji B aliangalia mchezo wa jana). Aidha, katika muktadha huu, KIPRA *mh* kinaonekana kusemwa kwa kiimbo cha kuitika kinachohusisha ruwaza za kupanda na kushuka huku kukiwa na mwendelezo kidogo wa sauti /m/ ilhali sauti /h/ ikiwa na msikiko hafifu. Pia, KIPRA *mh* katika muktadha huu kinatumika kama tamko linalojitegemea bila kuambatana na maneno mengine. Hivyo, kwa

kuzingatia muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kinachanua dhima ya kuitika.

Dhima ya kurudia kauli/swali

Data ya utafiti huu inaonesha kwamba KIPRA *mh* kilitumika pia kuashiria kwamba mzungumzaji anamtaka mshiriki mwingine wa mazungumzo arudie kauli aliyoisema awali au arudie swali alilouliza awali. Dondoo Na. 2 kutoka katika kijiwe cha mamantilie inathibitisha hilo:

Dondoo Na. 2:

8. A. ((anaita))We: Jane.
9. B. Abee
10. A. Mama Issa alikuja?
11. B. **M:h?**
12. A. Mama Issa alikuja hapa?
13. B. Hapana, hajaja.
14. A. Dah! sijui nitampataje maana napiga simu yake haipatikani....

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Tanga (2020)

Kwa kuchunguza dondoo hili, ni dhahiri kwamba KIPRA *mh* kinatumika kumtaka mzungumzaji arudie kauli aliyoisema awali au swali alilouliza awali (sawa na kusema, *umesema nini vile?*). Dhima hiyo ilionekana kujitokeza zaidi katika mazingira ambayo ama msikilizaji hajasikia kabisa kauli au swali lililoulizwa awali au amesikia kwa kiasi na hivyo, anataka kupata uhakika kama alichokisikia ni sahihi au la, ili naye atoe kauli/jibu sahihi kwa kauli au swali aliloulizwa. Ushahidi wa kimuktadha kwamba KIPRA *mh* kinachanua dhima hiyo unatokana na kitendo cha mzungumzaji A kurudia kile alichokisema awali (taz. mstari wa 12). Hata hivyo, imedhihirika kwamba KIPRA *mh* kilipotumika kubeba dhima hiyo, kilisemwa kwa kutumia kiimbo cha juu (kuashiria swali) huku sauti /m/ ikisemwa kwa mwendelezo kidogo tofauti na kilivyosemwa katika Dondoo

Na. 1 mstari wa 2 kilipochanua dhima ya kuitika. Hali hii inaonesha kuwa usemaji tofauti wa KIPRA *mh* ni kiashiria pia cha kimuktadha kinachosaidia kuchanua dhima za VIPRA. Aidha, ilibainika kwamba KIPRA *mh* kilipotumika kuchanua dhima hiyo kilijitokeza pia kama tamko linalojitegemea kama kilivyojitokeza katika muktadha wa kuashiria *kuitika*. Hivyo basi, katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kinachanua dhima ya kuashiria kurudia kauli au swali.

Dhima ya kudokeza kumpa mtu kitu/pokea

Utafiti huu ulibaini kwamba KIPRA *mh* kilitumika kumjulisha mshiriki mwingine wa mazungumzo kuwa apokee au achukue kitu. Dondoo Na. 3 inayohusu mazungumzo yaliyofanywa katika kijiwe cha mamantilie inabainisha dhima hiyo:

Dondoo Na. 3:

15. A.... ((Huku akimtazama mzungumzaji B)) Kaniletee kisu.

16. B. ((Anakwenda kuchukua kisu na kisha anarejea)) **m \bar{h}** ((anatamka *mh* huku akimpa kisu mzungumzaji A))

17. A. ((anachukua kisu kisha anaendelea na kazi.))....

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Dar es Salaam (2020)

Katika muktadha huu, mzungumzaji A anamtuma mzungumzaji B alete kisu. Mzungumzaji B anachukua kisu na kumpa mzungumzaji A huku akitumia KIPRA *mh* kuashiria kwamba apokee kisu hicho. Baada ya kutamka KIPRA hicho, mzungumzaji B anapokea kisu hicho na kuendelea na kazi. Hivyo, ni dhahiri kuwa KIPRA *mh* katika muktadha huu kimetumika kudokeza kumpa mtu kitu (sawa na kusema pokea).

Dhima ya kuanzisha mazungumzo

Katika miktadha mingine tofauti, KIPRA *mh* kilibainika kutumika kuanzisha mazungumzo. Dondoo Na. 4 kutoka katika kijiwe cha kahawa inathibitisha dhima hii:

Dondoo Na. 4:

18. A. ...((Anafika kijiweni na kuwakuta washiriki kadhaa wakinywa kahawa)) **mh:::** habari zenu jamani?
19. B. [[Njema]]
20. C. [[Salama tu]]
21. D. [[Nzuri shikamoo]]
22. A. ((Anajibu huku akimtaazama mzungumzaji D)) Marhabaa mama hujambo?
23. D. Sijambo.
24. A. Leo naona mambo mseto ati!
25. B, C na D ((wanacheka kwa pamoja))...

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Tanga (2020)

Mazungumzo katika dondoo hili yanaonesha kwamba mshiriki mmojawapo wa mazungumzo anafika katika kijiwe na kuanzisha mazungumzo huku akitumia KIPRA *mh* na kufuatiwa na salamu. Washiriki wengine wanajibu salamu, kisha mazungumzo mengine yanaendelea. Viashiria vya kimuktadha kama vile nafasi yake mwanzoni mwa tamko (Taz. Mstari wa 18) na kiimbo cha kuanzisha mazungumzo kinachohusisha mwendelezo zaidi wa sauti /h/ ni miongoni mwa viashiria vya kimuktadha vilivyosaidia kubaini dhima hiyo ya kuanzisha mazungumzo.

Dhima ya kuashiria jambo limefanywa kwa usahihi

KIPRA *mh* kilibainika pia kuashiria kuwa mshiriki mwingine wa mazungumzo amefanya jambo kwa usahihi. Dondoo Na. 5 kutoka katika mazungumzo ya mamantilie inathibitisha dhima hii:

Dondoo Na. 5:

26. A. Vipi pilau limeiva?
 27. B. Eh, limeiva.
 28. A. Ngoja tuone kwanza maana wewe hukawii kupika pilau bokoboko.
 29. B. Limeiva vizuri mama.
 30. A. (0.5) ((anachukua mpao na kuchota pilau kidogo, kisha anaonja))
Mh:::, hivi ndio unatakiwa kupika pilau, sio unajaza mimaji mpaka linakuwa bokoboko...
- Chanzo:** Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Tanga (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, dhima inayoonekana kuchanuzwa ni kuashiria kuwa mshiriki mwingine wa mazungumzo amefanya jambo kwa usahihi. Dhima hiyo inathibitika zaidi katika mstari wa 30 ambapo mara baada ya kutumia KIPRA hicho, mzungumzaji anasisitiza kwamba hivyo ndivyo anavyopaswa kupika pilau. Pia, KIPRA *mh* katika muktadha huu, kinasemwa kwa kiimbo cha kupatia kinachohusisha uendelezi wa sauti /h/ ilhali sauti /m/ ikiongezewa mkazo. Hivyo, ni dhahiri kwamba katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kimetumika kuashiria kuwa mshiriki mwingine wa mazungumzo amefanya jambo kwa usahihi (sawa na kusema, ‘sawasawa’, ‘hivyo hivyo’ au umepatia’).

Dhima ya kuonesha hali mbalimbali za kiakili

KIPRA *mh* kilionekana kutumiwa na wazungumzaji kuonesha hali mbalimbali za kiakili. Dhima hiyo ilijitokeza zaidi katika mazungumzo yaliyohitajia washiriki wa mazungumzo kufikiri, kukumbuka au kutafakari jambo. Ufafanuzi zaidi kuhusu dhima hii umetolewa katika sehemu zinazofuata.

Kutoka katika hali ya kutoelewa kwenda katika hali ya kuelewa

Ilibainika kwamba KIPRA *mh* kilitumiwa na washiriki wa mazungumzo kuonesha kwamba mzungumzaji anatoka katika hali ya kutokuelewa jambo kwenda katika hali ya kuelewa jambo hilo. Tuchunguze Dondoo Na. 6 kutoka katika mazungumzo yaliyofanywa katika kijiwe cha kahawa:

Dondoo Na. 6:

31. A. ((Anafika kijiweni)) Leo naona mambo mseto ati!
32. B, C na D ((wanacheka kwa pamoja)).
33. C. Kawaida tu, mbona siku hizi wanawake wengi tu wanakuja kunywa kahawa hapa.
34. A. Haya tufahamiane basi, mimi naitwa bwana Rajabu ((anataja jina huku akimwangalia mzungumzaji D)).
35. D. Naitwa Maria.
36. C. (0.5) Huyu ni mtafiti bwana. Amekuja kufanya utafiti hapa Tanga.
37. A. ((Huku akitikisa kichwa kutoka chini kwenda juu na kutoka juu kwenda chini)) **Mh::** ndio maana nimeona sura ngeni. Unatoka wapi mama? ((Anauliza huku akimwangalia mzungumzaji D))
38. D. Ninatoka Dar es Salaam.
39. A. ((Huku akitikisa kichwa kutoka chini kwenda juu na kutoka juu kwenda chini **Mh::**, karibu sana mama.
40. D. Asante sana...

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Tanga (2020)

Mazungumzo haya yalipochunguzwa, ilibainika kwamba mzungumzaji A hajui lolote kuhusu mshiriki mmojawapo wa mazungumzo, lakini mara baada ya kufafanuliwa anaelewa, na, hivyo, anatumia KIPRA *mh* kuashiria kwamba sasa ametoka katika hali kutoelewa kwenda kwenye hali ya kuelewa. Hata hivyo, ni vyema kusisitiza kuwa KIPRA *mh* kilipotumika kuchanua dhima hiyo kilisemwa kwa namna tofauti na kilivyosemwa katika miktadha mingine tuliyo kwisha kuibainisha. Katika muktadha huu, KIPRA *mh* kinasemwa katika namna ambayo sauti /h/ inasemwa kwa mwendelezo kidogo. Hali hii inaashiria kwamba kiimbo ni miongoni mwa viashiria vya kimuktadha vinavyosaidia kuchanua dhima za KIPRA *mh*.

Aidha, KIPRA *mh* kilipotumika kuashiria dhima hiyo, kilijitokeza mwanzoni mwa tamko huku mshiriki wa mazungumzo akitikisa kichwa kutoka chini kwenda juu na kutoka juu kwenda chini kama ishara ya kuelewa. Hivyo basi, muktadha wa matumizi kwa kuzingatia nini kimesemwa kabla au baada ya matumizi ya KIPRA hicho, kiimbo kilichotumika, nafasi kilimokaa na ishara ya mwili ya kutikisa kichwa vilisaidia kuchanua dhima hiyo ya kuashiria kwamba mzungumzaji ametoka katika hali ya kutoelewa na kwenda katika hali ya kuelewa.

Kuashiria kutoka katika hali ya kutokukumbuka kwenda katika hali ya kukumbuka

Data ya utafiti huu inaonesha pia kwamba KIPRA *mh* kina dhima ya kuashiria kwamba mzungumzaji anatoka katika hali ya kutokukumbuka kwenda kwenye hali ya kukumbuka jambo. Mazungumzo katika Dondoo Na. 7 yanathibitisha dhima hiyo:

Dondoo Na. 7:

41. A. ...Ile barabara imeshazidiwa.
42. B. Ipi?
43. A. Si hii ya kwenda Mbezi mpaka Kibaha.
44. B. **Mh::**, ile haifai kabisa yaani.
 - a. A. =Kabisa, sasa hivi unaweza tumia hata masaa manne hiki kipande cha kutoka kimara mpaka Kibaha...

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Dar es Salaam (2020)

KIPRA *mh* katika Dondoo Na. 7 mstari wa 44, kimetumiwa kuashiria kwamba mzungumzaji anatoka katika hali ya kutokukumbuka kwenda katika hali ya kukumbuka. Mazungumzo kabla na baada ya kutumia KIPRA *mh* na kiimbo cha kukumbuka kilichohusisha mwendelezo wa sauti /h/ (Mh::) ni miongoni mwa viashiria vya kumuktadha vilivyosaidia kubaini dhima hiyo.

Dhima ya jibu la swali

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, KIPRA *mh* kilitumiwa na wazungumzaji kama jibu la swali. Hata hivyo, tulibaini kwamba ingawa KIPRA hicho kilipotumiwa kuashiria jibu la swali, kuna tofauti ndogondogo za kidhima katika jibu la swali linalotolewa. Ufafanuzi zaidi kuhusu dhima hiyo unatolewa katika sehemu zinazofuata.

Jibu la swali linaloashiria kukubali au kuridhia ombi

KIPRA *mh* kulibainika kutumiwa kama jibu la swali linaloashiria kukubali au kuridhia ombi. Tuchunguze pia Dondoo Na. 46 na 47 zenye mazungumzo kutoka katika kijiwe cha kahawa na cha mamantilie:

Dondoo Na. 8:

45. A. Mwajuma jamani (°) si utanipa na mimi ‘dela’?

46. B. **Mh** nitakupatia.

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Dar es Salaam (2020)

Mazungumzo katika Dondoo Na. 8 yanaonesha kwamba mzungumzaji A anauliza swali akitaka kujua kama mzungumzaji B atampa vazi linaloitwa dela au la. Mzungumzaji B anatumia KIPRA *mh* kujibu swali akiashiria kwamba amekubali ombi la mzungumzaji A. Aidha, anathibitisha zaidi kuwa amekubali ombi hilo kwa kusema “nitakupatia” mara baada ya kutumia KIPRA *mh*. Vilevile, KIPRA *mh* kinasemwa kwa kiimbo cha maelezo kuashiria dhima hiyo. Hivyo, ni wazi kwamba KIPRA hicho kimetumiwa kama jibu la swali linaloashiria kukubali au kuridhia ombi.

Jibu la swali linaloashiria kukubali, kuthibitisha au kuthamini kile kilichosemwa

KIPRA *mh* kilionekana kutumika kama jibu la swali lililoashiria kukubali, kuthibitisha na kuthamini kile kilichosemwa na mzungumzaji mwingine. Dondoo Na. 9 kutoka katika kijiwe cha mamantilie inathibitisha dhima hii:

Data Na. 9:

48. A.Vipi pilau tamu e::h?

49. B. **M::h**(°) tamu kweli ((Huku akionesha sura ya furaha))

50. A. Umelipenda?=
51. B. =Sana. Najua mama Nansi huwa hufanyi makosa.

52. A. ((Anacheka)) Ha ha ha...

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Tanga (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, mzungumzaji A anamuuliza mzungumzaji B kama pilau ni tamu au la. Matumizi ya KIPRA *eh* chenye dhima ya kiangami-swali yanaashiria kwamba mzungumzaji anataka kupata uthibitisho kutoka kwa mzungumzaji B. Mzungumzaji B anajibu swali hilo huku akitumia KIPRA *mh* akiashiria kukubali au kuthibitisha kwamba pilau ni tamu. Ilibainika kwamba mzungumzaji B anakisema KIPRA hicho kwa kutumia kiimbo cha upole ilhali sauti /m/ ikisemwa kwa mwendelezo kidogo. Kiimbo hicho kinaashiria kwamba licha ya mzungumzaji kukubali na kuthibitisha, anathamini pia kile kilichosemwa Aidha, ilibainika kwamba KIPRA hicho kilitumiwa katika muktadha ambao mazungumzo ni ya kirafiki na yenye kuashiria upole huku wazungumzaji wakiwa na mwonekano wa sura za furaha. Hivyo, ni dhahiri kwamba katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kimetumika kuashiria jibu la swali linaloashiria kukubali, kuthibitisha na kuthamini kile kilichosemwa na mzungumzaji mwingine.

Jibu la swali linaloashiria kukataa

Katika miktadha mingine, KIPRA *mh* kilitumika kama jibu la swali linaloashiria kukataa (sawa na kusema, ‘hapana’). Dondoo Na. 8 kutoka katika kijiwe cha mamantilie inathibitisha dhima hiyo:

Dondoo Na. 10:

53. A.Watu wa manispaa walipita?
54. B. **Mhmm** ((Anajibu huku akitikisa kichwa))
55. A. Dah! bora, maana wanatuweka roho juu juu tu.
56. B. Kwani walitangaza kuwa watapita?
57. A. Mh! mwenzangu! Bwana afya hataki tupikie barabarani. Wanataka tufungue migahawa na tununue mahotipoti makubwa yale ya chakula. Sasa tutaweza wapi? Mitaji yenyewe ndiyo hii kidogo, uwezo hamna.
58. B. Mh!=
59. A. =Yaani tunakaa roho juu juu kama wakimbizi ndani ya nchi yetu wenyewe....

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Tanga (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kimetumika kama jibu la swali linaloashiria kukataa jambo. KIPRA *mh* kilipotumika kuchanua dhima hiyo, kilionekana kusemwa kwa namna ya kukirudia (mhmh). Aidha, kiziada lugha (kutikisa kichwa kuelekea kushoto na kulia na kutoka kulia kwenda kushoto) kilisaidia kuchanua dhima hiyo. Hivyo, ni dhahiri kwamba dhima tofautitofauti za KIPRA *mh* zinachanuzwa kulingana na muktadha.

Dhima ya kuonesha hisia za mzungumzaji

Katika miktadha mingine tofauti, KIPRA *mh* kilibainika kutumika kuashiria hisia tofautitofauti za mzungumzaji. Ufafanuzi kuhusu dhima hiyo unatolewa katika sehemu zinazofuata.

Kuonesha dharau

Data ya utafiti huu inaonesha pia kwamba KIPRA *mh* kilitumika kuashiria hali ya kudharau. Mazungumzo katika Dondoo Na. 11 kutoka katika kijiwe cha mamantilie yanadhihirisha hilo:

Dondoo Na. 11:

60. A.((Anataja jina)) ninunulie supu basi.
 61. B. (0.4) Sijatembea na hela hapa=
 62. A. =Si useme huna hela tu.
 63. B. Mimi nina hela chafu wewe. Sipendi tu kutembea na hela.
 64. A. **Mh::** huna lolote ((huku akionesha sura ya dharau)).
 65. B. Tunafanya maendeleo.
 66. A. Ha ha ha tusemba tuone hayo maendeleo...
- Chanzo:** Mazungumzo katika kijiwe cha mamantilie, Dar es Salaam (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kimetumika kuashiria hali ya kudharau kile kinachosemwa na mzungumzaji mwingine (taz. mstari wa 64). Muktadha wa mazungumzo kwa kuzingatia nini kimesemwa kabla na baada ya usemi uliobeba KIPRA *mh*, kiimbo kilichotumika (kiimbo cha dharau kinachohusisha mwendelezo wa sauti /h/) sawia na mwonekano wa mzungumzaji (uso wa dharau) vilitusaidia kubaini dhima hiyo. Kwa ujumla, ni dhahiri kuwa KIPRA *mh* kina dhima mbalimbali za kipragmatiki ambazo hudhihirika kulingana na muktadha kinamotumika.

Kuonesha mshangao

Kadhalika, katika muktadha mwingine tofauti ilibainika kwamba KIPRA *mh* kilitumika kuashiria mshangao. Dondoo Na. 12 kutoka katika kijiwe cha kahawa inathibitisha dhima hii:

Dondoo Na. 12:

67. A....Yaani jamaa akiamua tu kuongea anaongea tu.=
68. B. =E:h akiamua kuongea anaongea tu.

69. C. Yule akili zake anazijua yeye mwenyewe.
70. B. Jana basi akaamua kuongelea ile meli yake aliyoikamata kipindi chake. Dah! yaani jana ndio nilimwelewa . Anasema “MIMI nimekamata meli na ushahidi kabisa ina samaki zaidi ya milioni sita. Wenzetu wa Msumbiji wakatusaidia kui-‘target.’ Tumei-‘target’ ile meli tumeikamata, tumeivuta mpaka Dar es Salaam. Kufika Dar es Salaam tumetoa zile samaki tumewapa wanachuo, tumewapa magereza, tumewapa viongozi, tumewapa na masikini. Lakini kesi tumeshindwa:”
71. A. **Mh!** kwa nini? ((Anaonekana kushangazwa na taarifa hizo))
72. B. Kwa sababu gani:: wajanja Watanzania hawahawa kwa kushirikiana na wale wenye meli wameizamisha ile meli. Mpaka leo, tunashindwa kuitoa ili tutengeneze ushahidi. Lakini waliohusika kuizamisha ile meli ni WATANZANIA.
73. C. A::h, ina maana meli ilizama kweli?=
74. B. =Mpaka leo wanasema ipo hapo.
75. A. Imezama=
76. B. =Imezama
77. A. Kwa hiyo?=
78. B. =Tukakosa ushahidi, meli iliyokamatwa ipo wapi?
79. A. **Mh!** Ina maana ilikuja ikapiga nanga ikatoka?
80. B. E:h! Unaambiwa yaani mpaka leo ipo hapo kwenye kinu
81. A=Lakini wenyewe wanaiona?
82. B. NDIYO.
83. A. Kwa hiyo waki-‘dive’ wanaikuta ndani?
84. B. =Waki-‘dive’ wanaikuta ndani.
85. C. Sasa yeye kwa nini asiseme meli ipo hapa imezama?
86. B. Si Watanzania wanawasaidia kesi ili tushindwe wapate ‘mshiko!’
87. C. Kazi kwelikweli.
88. B. Anasema hakutoka mtu Norway wala hakutoka mtu Denmark. Ni Watanzania wenyewe kwa kushirikiana na viongozi wakazamisha meli wakijua serikali itashindwa.
89. A. **Mh!**
90. C. Ndiyo, kwa hiyo anasema dizaini kama hiyo ndiyo iliyosababisha hata viwanda kufa.
91. A. Dah! Kweli Watanzania tunaliwa...
- Chanzo:** Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Dar es Salaam (2020)

Katika muktadha huu wa mazungumzo, KIPRA *mh* kilionekana kutumika kuashiria mshangao. Hii ina maana kwamba mzungumzaji anashangaa kutokana na taarifa anazosisikia kwani taarifa hizo zinaonekana ni mpya kwake. Ilibainika kwamba KIPRA *mh* kilipotumika kuchanua dhima hiyo, kiliweza kujitokeza ama mwanzoni mwa tamko (taz. mstari wa 71 na 79) au kilijitokeza peke yake kama tamko linalojitosheleza kimaana (taz. mstari wa 89). Kwa ujumla, viashiria vya kimuktadha kama vile taarifa zilizosemwa kabla na baada ya matumizi ya KIPRA hicho, kiimbo cha mshangao kilichotumika, nafasi kilimokaa na viziada lugha (mwonekano wa sura ya kushangaa) vilisaidia kuchanua dhima hiyo. Hivyo, ni wazi kwamba katika muktadha huu wa mazungumzo KIPRA *mh* kinachanua dhima hiyo ya mshangao.

Dhima ya kuruhusu kuendelea kuzungumza

Utafiti huu ulibaini kwamba KIPRA *mh* kilitumiwa katika mazungumzo kuashiria kwamba mzungumzaji anamruhusu mshiriki mwingine wa mazungumzo aendeleo kuzungumza. Tuchunguze pia Dondoo Na. 13 inayohusu mazungumzo yaliyofanyika katika kijiwe kimojawapo cha kahawa:

Dondoo Na. 13:

92. A. Hizi ajali za pikipiki hizi ni balaa. Unamkumbuka yule Jose?
93. B. **Mh** ((huku akitikisa kichwa kutoka chini kwenda juu))
94. A. Alipata ajali bwana. Basi kwenda kwa 'dokta' wacha amtukane.=
95. B. =**Mh!**
96. A. Ikabidi amwombe dada yake ambaye ni nesi alisomea hapahapa akambembeleze 'dokta'.
97. B. =**Mh:õ**
98. A. Ndio dokta kukubali=
99. B. =**Mh:õ**
100. A. Aliporudi kwa dokta akamwambia kuna foleni.=
101. B. =**Mh:õ**

102. A. Kaka wiki zima.
103. B. Foleni?
104. A. Eh, kaambiwa kuna foleni.
105. B. Aisee!
106. A. Haya kuja kufanyiwa oparesheni sasa keshaoza. Kumbe kaumia vibaya kawekewa hadi vyuma yaani.
107. B. Mh!
108. A. Baada ya kufanyiwa kaka siku ya kwanza, ya pili, ya tatu ule mshono ukafumuka ikabidi wafumue tena waanze upya. Mpaka leo yupo huko. Tunakwenda kumuona.
109. B. Aisee! Wanasumbua sana hawa madaktari.
110. A. Mh wanasumbua sana.
111. B. Tatizo letu sisi Watanzania hatupendani. Watu wanaringa sana.=
112. A. =M:h wanaringa sana.
113. B. Sasa pale si unacheza na uhai wa mtu?=
114. A. =M:h unachezea kifo hapo.
115. B. Unajua, binadamu hatuwezi kufafanana. Kama Mungu kakupa karama hiyo basi itumie vizuri, sio kuwanyanyasa watu.=
116. A. =Ndiyo!
117. B. Sio unatumia kama fimbo kunyayasa wenzio inakuwa haipendezi.
118. A. =M::h haipendezi kabisa.
119. B. Lakini zamani mbona hazikwepo hizi ajali za pikipiki?
120. A. Zilikwepo, sema nini unajua, pikipiki zilikuwa chache
121. B. Sasa wao madaktari si inabidi waongeze utaalumu?=
122. A. =M::h inabidi waongeze ujuzi.....

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha kahawa, Tanga (2020)

Mazungumzo katika Dondoo Na. 13 yanaonesha kwamba KIPRA *mh* kimetumika kuashiria kwamba mzungumzaji anamruhusu mshiriki mwingine wa mazungumzo aendelee kuzungumza. Ilibainika kwamba mzungumzaji B anatumia KIPRA *mh* mara baada ya mzungumzaji A kumaliza kuzungumza ili kuashiria kwamba mzungumzaji huyo aendelee kuzungumza na pia mzungumzaji anaashiria shauku ya kutaka kusikia

kinachosemwa (Taz. mstari wa 97, 99 na 101). Dhima hiyo inalingana na ile ya kumueleweshwa mshiriki wa mazungumzo kwamba msikilizaji yupo pamoja na mzungumzaji, na, hivyo, aendelee kuzungumza kama ilivyoainishwa na Pipek (2007). Viashiria mbalimbali vya kimuktadha kama vile kitendo cha mzungumzaji mwingine kuendelea kuzungumza mara tu baada ya kuruhusiwa kwa kutumia KIPRA hicho, kasi ya mazungumzo na kiimbo cha hamasa kilichotumika vinaashiria kwamba mzungumzaji B ana hamasa ya kutaka kujua zaidi kuhusu kile kinachosemwa. Kwa ujumla, KIPRA *mh* katika muktadha huu wa mazungumzo kimetumika kuashiria kwamba mzungumzaji anamruhusu mshiriki mwingine wa mazungumzo aendelee kuzungumza lakini pia anaashiria hamasa ya kutaka kujua zaidi kuhusu kile kinachosemwa.

Hitimisho

Kutokana na data yetu na uchambuzi tulioufanya, ni wazi kwamba KIPRA *mh* kina dhima mbalimbali za kipragmatiki. Dhima zinazochanuzwa na KIPRA hicho hutegemea namna kilivyotumiwa katika muktadha wa mazungumzo kwa kuzingatia nini kimesemwa kabla na baada ya KIPRA hicho, nafasi ambamo KIPRA hicho kimekaa katika tamko, kiimbo kilichotumika na ishara za mwili zilizoambatana na usemaji wa KIPRA hicho. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini dhima 9 tofauti za KIPRA *mh* ambazo ni: kuashiria kuitika, kumjulisha mshiriki mwingine wa mazungumzo arudie kauli au swali, kuashiria kwamba mhusika apokee au achukue kitu, kuanzisha mazungumzo, kuashiria kwamba jambo

limefanywa kwa usahihi, kuonesha hali mbalimbali za kiakili, kutumika kama jibu la swali, kudokeza hisia mbalimbali na kumruhusu mshiriki mwingine wa mazungumzo aendelee kuzungumza. Hata hivyo, ni vyema kuweka wazi kwamba dhima za KIPRA *mh* tulizozijadili hapa ni kwa mujibu wa vyanzo viwili tu vya data: vijiwe vya kahawa na vijiwe vya mamantilie. Upo uwezekano wa KIPRA *mh* kuwa na dhima nyingine zaidi ya tulizozijadili katika makala haya kama uchunguzi wa kina zaidi utafanyika.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yanatofautiana na tafiti za awali kama vile za Pipek (2007), BAKIZA (2010), TUKI (2012), BAKITA (2017) na Kibiki (2019b) kwani utafiti huu umebainisha dhima tofauti na zilizokwisha bainishwa katika tafiti hizo za awali. Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yanadokeza kwamba VIPRA vina dhima mbalimbali katika lugha ya Kiswahili na ni eneo ambalo linadokeza utajiri wa kiutafiti katika uwanja wa kipragmatiki. Tunapendekeza tafiti zaidi zifanyike kuchunguza VIPRA vingine katika lugha ya Kiswahili ili kubaini dhima zake. Aidha, kialami pragmatiki *mh* kinaweza kuchunguzwa zaidi kwa kuhusisha na taaluma za fonolojia na fonetiki ili kubaini ruwaza zake na athari zake kwenye maana za kialami hicho.

Marejeleo

BAKITA, (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili* (Toleo la Pili). Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Baumann, S na Grice, M. (2006). Intonation of Accessibility. Katika *Journal of Pragmatics*. 38, 1636 - 1657.

- Egan, O. (1980). Intonation and Meaning. Katika *Journal of Psycholinguistics*. 9 (1), 23 - 39.
- Fraser, B. (1999). What are Discourse Markers? Katika *Journal of Pragmatics*. 31, 931 - 952.
- Fung, L na Carter, R. (2007). Discourse Markers and Spoken English: Native and Learner Use in Pedagogical Settings. Katika *Applied Linguistics*. 28 (3), 410-439.
- Goodness, D. (2020). The Form 'sasa' as both a Temporal Adverb and a Discourse Marker in Kiswahili. Katika *Kiswahili*. 83, 130 - 146.
- Gumperz, J. (1982). *Discourse Strategies*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Halliday, M.A.K. (1994). *An Introduction to Functional Grammar* (Toleo la Nne). London: Edward Arnold.
- Kawulich, B.B. (2006). Participant Observation as a Data Collection Method. Katika Forum: Qualitative Social Research. <http://www.qualitative-research.net/fqs/>. Iliyosomwa 25 Mei, 2019.
- Kibiki M.J. (2019b). Mchango wa Ishara za Mwili kwenye Maana katika Lugha ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Vialami Pragmatiki *eh, sawa, mh* na *ah*. Katika *JULACE*. 4 (2), 67 - 86.
- Kibiki M.J. na Malangwa, P.S. (2018). Dhima za Kipragmatiki za Kialami Pragmatiki *ah* katika Kiswahili cha Mazungumzo. Katika *JULACE*. 3(2), 53 - 73.
- Kibiki M.J. na Malangwa, P.S. (2019a). Dhima za Kipragmatiki za Kialami Pragmatiki *eh* katika Kiswahili cha Mazungumzo. Katika *Mwanga wa Lugha*. 2 (2), 13 - 30.
- Kibiki M.J. na Malangwa, P.S. (2019b). Athari za Kiimbo kwenye Maana za Kialami Pragmatiki *eh* katika Mazungumzo ya Kiswahili. Katika *Jarida la Kimataifa la Isimu ya Kibantu*. 2(2): 62 - 78.

- Kibiki, M.J. (2019a). The Pragmatic Functions of the Marker *sawa* in Spoken Swahili. *Katika Studies in African Languages and Cultures*. 53, 29 - 55.
- Kreidler, C.W. (2002). *Introducing English Semantics* (Toleo la pili). London. Routledge.
- Kreswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative and mixed methods approaches* (Toleo la 4). New Dehl: SAGE Publications India Pvt. Limited.
- Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. & Msanjila, Y.P. (2013). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Marjie, S. & Sosoo, F.K (2021). The Communicative Functions of 'yaani' on Tanzania WhatsApp Platforms. *Katika Ghana Journal of Linguistics*, 10 (1), 305 - 328.
- Pipek, V. (2007). On Backchannels in English Conversation, (Tasinifu ya Diploma, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Masaryk. Iliyosomwa 19/08/2019 kutoka <https://is.muni.cz/th/f75c5/Diploma.Thesis.pdf>.
- Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Psathas, G., & Anderson, T. (1993). The Practices of Transcription in Conversation analysis. *Katika Semiotica*. 78 (1 & 2), 75 - 99.
- Redeker, G. (1991). Review Article: Linguistic Markers of Discourse Structure. *Katika Linguistics*. 29, 1139 - 1172.
- Schiffirin, D. (2001). Discourse Markers, Language, Meaning and Context. *Katika D. Schiffirin., D. Tannen na H. E. Hamilton. The Handbook of Discourse Analysis*. Uk. 54 - 75. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.
- Snow, D & Balog, H. (2002). Do Children Produce the Melody Before the Words? A Review of Developmental Intonation Research. *Katika Lingua*. 112, 1025 - 1058.

Susan, D. A. (1999). *The Pragmatics of Selected Discourse Markers in Swahili* (Tasinifu ya Uzamivu, haijchapishwa), Chuo Kikuu cha Illinois. Iliyosomwa 23/06/2019 kutoka <https://www.ideals.illinois.edu/handle/2142/20068>.

TUKI. (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.*, Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.

Van Bergen, G & Degand, L. (2018). Discourse Markers as Turn-transition Devices: Variation in Speech and Instant Messaging. *Katika Discourse Strategies*. 55 (1), 47 - 71.

Kiambatisho

Alama za Unukuzi Zilizotumika na Maana Zake

Alama Zilizotumika kwa Mujibu wa Psathas na Anderson (1990)	
ALAMA	MAANA
1, 2, 3, 4,5,6 na kadhalika	Namba ya sentensi au zamu tofauti za kuzungumza
A, B, C	Kuwakilisha majina ya wazungumzaji
Herufi kubwa katika silabi au neno (Mfano, SAWA)	Maneno yaliyosemwa kwa kuongezeka kwa sauti kuashiria msisitizo
(())	Kufafanua matendo yanayofanywa na washiriki wa mazungumzo
=	Mfululizo wa uzungumzaji; mzungumzaji wa pili ameanza kuzungumza mara tu baada ya mzungumzaji wa kwanza kumaliza au mzungumzaji huyohuyo ameongea jambo moja na kisha akaongea jambo jingine bila kupumzika
Namba zilizowekwa katika mabano, kwa mfano (0.5)	Muda wa ukimya (katika sekunde)
[[]]	Mazungumzo yanayotokea kwa wakati mmoja (wazungumzaji wawili au zaidi wanaanza kuzungumza kwa wakati mmoja)
:	Kiwango cha urefushaji wa silabi. Nukta pacha zitaongezeka au kupungua kutegemea na kiwango cha

Alama Zilizotumika kwa Mujibu wa Psathas na Anderson (1990)	
	urefushaji wa silabi husika
—	Mstari unaowekwa chini ya neno au silabi umetumika kuashiria mkazo (mfano: <u>Wewe</u>)
—	Mstari unaowekwa juu ya neno (mfano: mh) umetumika kuashiria kiimbo cha maelezo.
(°)	Imetumika kuashiria sauti inayotamkwa kwa kubembeleza au kwa upole
,	Kiimbo cha kuendelea
?	Kiimbo cha swali
!	Kiimbo cha mshangao
...	Baadhi ya mazungumzo yameondolewa
-	Mstari unaowekwa baada ya neno, silabi au sauti kuashiria kwamba neno, silabi au sauti hiyo ilisemwa kwa kukatiza (mfano mi- badala ya mimi)
Alama za Unukuzi Zilizoongezwa na Watafiti	
..	Kiimbo cha kukasirika
ō	Kiimbo cha hamasa ya kutaka kusikia
Ō	Kiimbo cha dharau
Ō	Kiimbo cha hamaki
!ō	Kiimbo cha kushangaa na kuhamaki
!ō?	Kiimbo kinachoashiria kwamba mzungumzaji anashangaa, anahamaki lakini pia anauliza swali
ō	Kiimbo cha hamasa ya kutaka kusikia jambo